

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



MKUTANO WA MASHAURIANO WA WADAU JUU YA UJENZI WA KIWANDA CHA MBOLEA KWA KUTUMIA MALIGHAFI YA TAKA KATIKA ENEO LA MABWEPANDE MANISPAA YA KINONDONI DAR ES SALAAM TAREHE 31/08/2017.


Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inakusudia kujenga na kiwanda cha mbolea katika eneo la Mabwepande Wilaya ya Kinondoni Dar es salaam kitakachotumia malighafi ya taka za kwenye masoko. Mradi huu unafadhiliwa na Jiji la Free and Hanseatic City Hamburg – Ujerumani lenye mahusiano na Jiji la Dar es Salaam.

Ujenzi wa mradi huu unatarajia kuanzia mwezi Septemba, 2017. Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, washirika wa mradi na taasisi isiyo ya Kiserikali ya 'atmosfair gGmbH' wanapenda kukualika kwenye mkutano wa wadau juu ya ujenzi na uendeshaji wa mradi huu.

Lengo kuu la mkutano huo ni kujadiliana na wadau mbalimbali namna ya kuufanya mradi kuwa endelevu na wenye kuzingatia hali ya mazingira.

Mkutano huu utafanyika siku ya Alhamisi tarehe 31/08/2017 kuanzia Saa 4:00 asubuhi katika Ukumbi wa Manispaa ya Kinondoni uliopo Ofisi Kuu za Manispaa eneo la Magomeni kwenye makutano ya barabara za Morogoro na Kawawa.

Wadau wote walioalikwa wanaombwa kushiriki ili kufanikisha mkutano huu muhimu.



Aron T. Kagurumjuli

MKURUGENZI WA MANISPAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI